TAARIFA HALISI NAMBA KUMI

"VIPENGELE VINNE VIKUBWA VINAVYOCHOCHEA KUENEA KWA UKIMWI"

1. Vipengele vya Kiuchumi na Umaskini

VVU si matokeo ya umaskini, bali umaskini huongeza hatari ya maambukizi ya VVU, na VVU/UKIMWI huzidisha umaskini na njaa.

Afrika ina viwango vya juu vya umaskini na matokeo ya kiwango cha juu ya VVU/UKIMWI duniani. Kwa mujibu wa benki ya Dunia wastani wa asilimia 46 hadi asilimia 76 ya watu wa Afrika wanaishi chini ya kiwango cha umaskini.

Katika miaka ya 1980, wakati janga la VVU/UKIMWI lilipoanza kujitokeza, lilikuta hali nzuri ya kujiimarisha katika Nchi za Afrika, kusini mwa jangwa la Sahara. Nchi nyingi zilikuwa zikijitahidi kukabili matatizo ya kijamii na kiuchumi, ikiwemo kasumba ya ukoloni kama vile umaskini wa umma, na miundombinu michache ya elimu na afya. Matakwa ya marekebisho ya muundo na mzigo mkubwa wa deni la Afrika viliathiri sana utoaji wa huduma za jamii zikiwemo miundombinu ya afya. Ukame na njaa vinavyojirudia viliathiri watu na kuleta vifo, hasa ukame uliozikumba nchi 20 za Afrika mwaka 1984 – 1989. Nchi za Afrika, baada ya miaka 10 hadi 20 ya uhuru zimekabiliwa na kupungua kwa bei za mazao ya msingi na kuongezeka kwa bei za mafuta. Nchi nyingine zilikuwa bado zinapigania uhuru. Hali katika nchi nyingine bado kuna migogoro, kugombea madaraka na rushwa vimeathiri utulivu na kupanua tofauti baina ya watu na umaskini.

Kukabiliana na shinikizo hizi na mahitaji mengi ya maendeleo huku kukiwa na rasilimali chache za taifa, na kushughulikia miundombinu michache ya mawasiliano na afya, nchi zilijikuta na uwezo mdogo wa kupambana na VVU tangu mwanzo. Vipengele vya kijamii na kiutamaduni vilivyopo katika sehemu kubwa ya Afrika, na kutokuwa tayari kukiri kwa uwazi na kukabili magonjwa ya sababishwayo na ngono kwa kiwango kikubwa nao umevipa Virusi Vya UKIMWI umaarufu.

Nchi nyingi ambazo asilimia moja tu ya watu ndio walioambukizwa VVU miaka 15 iliyopita, hivi sasa zina kiwango cha ueneaji wa VVU cha asilimia 10 au zaidi, huku wale wote walioathirika kuwa maskini zaidi katika jamii.

Uchambuzi wa uhusiano kati ya vifo vinavyohusiana na UKIMWI na umasikini/njaa Kusini mwa Afrika umeonyesha uhusiano ufuatao:

- Kaya zisizokuwa na mtu mzima anayezalisha mali zilikuwa na mapato pungufu kwa asilimia 31 kuliko kaya zenye watu wazima wanaozalisha mali.

- Kaya zenye watu wazima wawili mahututi zilikuwa na mapato pungufu kwa asilimia 66 kuliko kaya zisizokuwa na watu wazima mahututi.

- Familia za Zambia ambazo Mkuu wa kaya alikuwa mahututi zililima mazao pungufu kwa asilimia 53 kuliko kaya zisizokuwa na watu wazima mahututi.

- Kifo cha mwanafamilia mmoja aliyepata mshahara nchini Cote d'Ivoire kimepunguza wastani wa mapato ya kaya kwa zaidi ya nusu.

- Wajane na yatima mara nyingi hunufaisha wanafamilia na watu wengine. Kwa mfano wanawake na watoto mara nyingi wanapoteza nyumba zao na ardhi mara mume/baba anapofariki, iwe kwa ndugu wa familia yake au watu wa nje wanaoona fursa ya kupora mali.

- Haja ya kuishi katika mazingira ya namna hiyo mara nyingi hulazimisha wanawake maskini sana na watoto kujishughulisha zaidi katika shughuli hatarishi kwa maambukizi ya VVU (kwa mfano biashara ya ngono).

Watu maskini wana upungufu wa lishe na wanapata huduma za afya hafifu/chache au wanakosa kabisa. Lishe duni huzidisha VVU na bila matunzo ya mara kwa mara, dalili za VVU hubakia bila kutibiwa na kuongeza hatari ya maambukizo ya VVU.

Umaskini pia unahusiana na kiwango cha juu cha matukio ya maradhi. Katika nchi nyingi za Afrika, malaria, kichocho, tegu na kifua kikuu huongeza urahisi wa maambukizo ya VVU.

Kutokomeza umaskini, njaa na maradhi yanayoweza kuzuiwa ni muhimu sana kwa juhudi za kuzuia VVU/UKIMWI.
Kuharakisha uzuiaji wa VVU kutasaidia kupunguza umaskini zaidi.
Utokomezaji umaskini na kupambana na VVU/UKIMWI ni malengo ya maendeleo ya Milenia, mafanikio ya lengo moja huleta ufanisi wa lengo jingine.

2. Vipengele vya Elimu na Habari

Huduma za elimu mara nyingi haziwafikii watu maskini na wanaoishi maeneo ya pembezoni barani Afrika. Hata hivyo utafiti umeonyesha kuwa iwapo watoto wote wamepata elimu kamili ya msingi, kiasi cha maambukizo mapya milioni 7 ya VVU yanaweza kuzuiwa katika mwongozi mmoja.

Wasichana wana uwezekano mdogo wa kupata elimu, kwa sababu wanatarajiwa kubaki nyumbani na kusaidia shughuli za nyumbani, kulea watoto na kuwatunza wagonjwa katika familia. Hata hivyo wasichana wanaomaliza elimu ya msingi wana uwezekano mkubwa wa kupata maarifa na stadi zinazohitajika kuepuka maambukizo ya VVU kuliko wengine, tafiti zimeonyesha hivyo.

- Utafiti katika nchi 11 umeonyesha kuwa **wanawake wenye elimu walikuwa na uwezekano wa mara tano wa kutumia kondomu sawa na wanawake wasio na elimu, mara ya mwisho walipofanya ngono.**

- Nchini Rwanda, wanawake wenye elimu ya Sekondari au zaidi walikuwa na uwezekano wa mara tano wa kujua njia kuu za maambukizi ya VVU kuliko wale wasio na elimu rasmi.

- Utafiti katika nchi 17 za Afrika umeonyesha kuwa wasichana wenye elimu zaidi wameelekea kuchelewa kufanya ngono na walikuwa na uwezekano mkubwa wa kusisitiza kuwa wenzi wao watumie kondomu.

- Vyanzo vya kawaida vya taarifa, ukiacha redio, havipo kwa watu wengi wa Afrika, na katika nchi nyingi viwango vya kutojua kusoma na kuandika ni vikubwa, na hivyo kukwaza matumizi ya ujumbe na taarifa za maandishi.

- Ujumbe na njia za mawasiliano zinazofaa kwa kufikishia zinafaa kuendelezwa, kwa sababu bila ya taarifa sahihi, watu hawawezi kuelewa kwa ukamilifu maana ya VVU/UKIMWI, namna unavyoenezwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine na namna ya kuzuia kuenea kwake.

- Utafiti wa hivi karibuni nchini Botswana umegundua kuwa pamoja na juhudi kubwa za elimu ya VVU, asilimia 77 ya wale waliofanyiwa utafiti wamedhani kuwa Virusi Vya UKIMWI vinaenezwa na mbu.

3. Vipengele vya Kijamii

Vipengele viwili muhimu vya kijamii vinavyochochea kuenea kwa UKIMWI ni pamoja na **hadhi ya chini ya wanawake na viwango vikubwa vya maambukizi miongoni mwa watoto na vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24** barani Afrika. Mada hizi zimejadiliwa katika makala nyingine na hasa katika makala ya 8 na 9.

Aidha kuhusiana na kuenea kwa VVU ni **mifumo ya ajira na uhamaji wa watu katika Nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara,** ambalo mipaka ya wazi, ghasia, migogoro na matarajio mabaya ya uchumi, vikichanganywa pamoja huwafanya watu waache familia na jamii zao kwenda kutafuta maisha. Kusafiri safari ndefu, sekta ya madini, na kilimo cha mashamba makubwa ni mifano ya hali ambayo kuenea kwa VVU kumechochewa wakati watu wanapotengwa na misaada ya kimila katika mazingira yaliyojitenga.

Hadhi ya chini ya wanawake na wasichana katika jamii nyingi na viwango vya chini vya stadi, elimu na fursa chache za ajira husababisha biashara ya ngono kuwa njia ya mwisho kutumiwa kujipatia kipato. Hiki pia ni kipengele kingine cha kijamii kinachohusu hukosekana kwa usawa wa kijinsia kunakoonekana na kunakochangia kuenea kwa VVU. Aidha kuhusiana na hayo ni matukio mengi ya talaka na

mitara, yanayowafanya wanawake wawe hatarini zaidi kuambukizwa VVU na yanayowalazimisha kufanya biashara ya ngono.

Unyanyapaa na ubaguzi ni vichocheo vikubwa vya kuenea kwa VVU. Utesaji na unyanyasaji wanaofanyiwa watu wengi wanaoishi na VVU na UKIMWI na familia na jamii zao, huwafanya watu wengi washindwe kujua hali zao; kuathiri juhudi za kutoa huduma za upimaji, unasihi na matibabu na hivyo hatimaye kuathiri uzuiaji wa maambukizi ya VVU.

Fikra potofu kuhusu VVU, (hasa dhana kwamba ni aina ya maapizo na adhabu kutoka kwa Mungu kutokana na tabia mbaya) huchangia sana unyanyapaa katika jamii nyingi za kiasili Barani Afrika.

Utafiti uliofanywa mwaka 2005 nchini Afrika Kusini umebaini kuwa uvumilivu kwa watu wanaoishi na VVU au UKIMWI ni mkubwa sana katika maeneo ya mijini kuliko vijijini. Matokeo hayo yanamaanisha kuwa kufahamika kwa ugonjwa kunaufanya uonekane wa "kawaida", na hivyo kupunguza imani na desturi za ubaguzi.

4. Vipengele vya utamaduni

Matambiko na taratibu nyingi za utamaduni, zikiwemo tohara, ukeketaji na mila na desturi nyingine **zinazohusu utoaji kafara** ("sadaka ya tambiko") huwasababishia wanaoshiriki kuwa hatarini iwapo vitafanywa katika mazingira yasiyotakaswa, ambayo hutokea sana katika maeneo ya vijijini. Matambiko na sherehe zinazohusiana na kubalehe/kuvunja ungo vina mwelekeo pia wa kuongeza kasi ya hatari ya ngono na ubakaji. **Nchini Tanzania, vijana wamechunguza vipengele hatarishi vya VVU katika jamii zao na kufanikiwa kuwalalamikia viongozi wa Wilaya waongeze udhibiti mkali zaidi wa matambiko na sherehe.**

Ndoa za mapoma, zinazohusiana na nafasi ya kijinsia aliyonayo mwanamke katika jamii, zinachochea hatari ya wasichana kuambukizwa VVU. Wanawake vijana wako hatarini zaidi kimaumbile kuambukizwa na hawawezi kujadiliana kuhusu ngono salama na waume wao watu wazima. Utafiti umeonyesha kuwa wanawake vijana walioolewa wana uwezekano mkubwa wa kuambukizwa VVU kuliko wale wasioolewa.

Kuwapeleka watoto kufanya kazi mijini kwa ajili ya ndugu zao ("kulea") pia huwafanya wawe hatarini kuambukizwa, hasa kutokana na mateso wanayopata huwafanya wakimbie na kuishi mitaani.
Baadhi ya mila na desturi zinalazimisha kwamba, anapofariki mume, mjane moja kwa moja anakuwa mke wa shemeji yake. Iwapo mume amefarika kwa ugonjwa wa UKIMWI, desturi hiyo huwaweka ndugu na mke wake mwingine au wake, katika hatari ya kuambukizwa VVU.